# JE, USHIRIKIANO WA JAMII

## (CE) katika Maji na Usafi (WASH) ni nini?

**Kusudi a jumla la huduma ya Oxfam WASH wakati wa hali ya dharura ni kupunguza hatari za kiafya kwa umma kuhusiana na maji, usafi wa mazingira na afya.**

### Hii inamaanisha nini kihalisi?

Inamaanisha kufanya kazi moja kwa moja zaidi na idadi kubwa ya watu walioathiriwa na janga hilo ili kuwaelewa vizuri, kuwahimiza kufanya mabadiliko mazuri ya tabia, na kuimarisha uwezo wao wa kupunguza/kuzuia hatari za kiafya kwa umma na kufanya maamuzi yao wenyewe. Tunaita kazi hii ushirikiano wa kamii (CE).

## Ni Tofauti, bali Si Mpya.

CE katika WASH sio jambo jipya. Ushirikiano wa Jamii daima umekuwa msingi wa utejakazi wa dharura katika mipango ya Oxfam WASH. Walakini, mwenendo tunaotumikia ni tofauti, kwani tunasitizita zaidi upangaji wa mapema na lengo kubwa la kuunda uaminifu katika idadi ya watu walioathiriwa na janga ili kuwaweka katikati ya mpango wetu wa WASH.

## Je, CE ni mpya kwa Oxfam?

Kwa utelekezaji, hii inajumuisha mtangamano endelevu na mashauriano yanayofaa na vikundi tofauti vya jamii yanayohusiana na vituo na huduma za WASH, kushughulikia matatizo yao kwa wakati unaofaa, na kutoa maoni ya mabadiliko yote yaliyofanywa.



**Kanuni za CE sio mpya kwa sekta ya misaada ya kibinadamu.**

Katika WASH, kanuni hizi hutolewa kutoka sekta mbalimbali lakini zinalenga njia ya pamoja, badala ya ulengaji katika boma. Kwa kuzingatia kwamba WASH inahitaji kutumika kwa wote na inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa kueneainaposhughilikiwa vibaya, ni muhimu kuwashirikisha watu wengi iwezekanavyo katika mpango huu.

CE katika WASH ni mchanganyiko wa elimu ya magonjwa ya mlipuko, afya ya umma, anthropolojia na uhamasishaji wa afya, unaolenga kubadilisha huduma kulingana na mahitaji ya kipekee ya kila jamii.

*"...tulikabiliwa na vifo vingi katika mitaa ya Butsili kwa sababu ya kutoaminiana kati yetu na timu ya kupambana na Ebola ...Oxfam iliwasiliana na mimi na kunielezea jinsi wanahusika katika mapambano hayo ... Baada ya kuhudhuria mkutano wa elimu, nilianzisha mikutano na viongozi wa jamii yangu ili kujadili jinsi ya kupambana na ugonjwa huu. Tulikuwa tukipokea wageni na kuzika wafu bila kuthibitisha hali yao ya kiafya, lakini sasa hatufanyi hivyo tena."*

**KAMBALE MUSANJALIRA JOSUÉ, MKUU WA MTAA, KIVU KASKAZINI, DRC**

## Kwa nini imani ni muhimu sana?

**Watu wanawezaje kuhamasishwa kubadilisha tabia zao ikiwa hawaamini kuwa hatua mpya zitaleta mabadiliko?**



- Inapohusu milipuko ya magonjwa, daima watu watakuwa na mbinu zilizopo za kukabiliana nayo. Tunataka kuimarisha uwezo uliopo, sio kuubadilisha na ufahamu wetu wenyewe.
- Tunataka kuwawezesha watu kuishi kwa kawaida iwezekanavyo licha ya mabadiliko makubwa katika maisha yao; hii inamaanisha kuelewa yale yaliyokuwa ya kawaida kabla ya tatizo, na kuunga mkono mabadiliko ya kurudi kwenye uzoefu huo, na maboresho yaliyokubaliwa.
- Tunataka kuongeza kukubalika na kuaminika kwa shughuli zetu za WASH, kwa kutumia maoni ya jamii kufanya mabadiliko yanayofaa kwa wakati kwenye programu zetu.

Kupata maelezo zaidi, angalia Mwongozo wetu wa Utangulizi wa CE katika WASH, na Jarida la Kutoa Rasilimali la CE.
Waweza kuzipata zote mbili kwenye mtandao
*bit.ly/CommunityEngagementinWASH*

OXFAM

## Mbintu yetu ya CE ni tofauti aje sasa?



**Awali...** Jamii ziliwekwa katika mipango yetu ya WASH.



**Sasa...** Tuna uwezo saidi wa kubadilika , kujizoeza Kuwa wasikivu kwa kuwaweka watu mbele (kuunda nafasi ya kusikiliza na kuelewa, badala ya kuongea na kupuuza).

### HATARI

**AWALI** Uendeshaji wa tathmini za hatari za haraka, tukiwa na nyaraka chache sana.

**SASA** Utegemezi mkuu katika data yakinifu (iliyokusanywa kwa kushirikiana na jamii), na mchakato unaoendelea wa kukusanya/ kuunda kulingana na maelezo yaliyokusanywa yanayohusiana na hatari, kinyume na hafla ya tukio moja mwanzoni mwa hali ya dharura.

### UJUMUISHAJI

**AWALI** Kushauriana na vikundi vya idadi ya watu walio hatarini kuhusu vipaumbele na mapendeleo yao lakini kusisitiza mwingiliano wote unaoendelea karibu na vikundi vya 'jamii inayoonekana' na tabala la wasomi wa kawaida.

**SASA** Kuhakikisha mtangamano unaoendelea na jamii tofauti – hasa vikundi vya watu walio katika hatari na watu waliotiwa pembezoni – kujumuisha na kuboresha ubora wa vifaa na huduma za WASH.

### MAWASILIANO

**AWALI** Matumizi ya njia anuwai za mawasiliano lakini kupitia mfumo mkubwa uliokusudiwa kufundisha (kuwaambia watu mambo ya kufanya).

**SASA** Kuunda nafasi ya kusikiliza na:

- msisitizo mkubwa wa mawasiliano ya pande mbili;
- uwezo wa kubadilika;
- uaminifu na uwazi katika viwango vyetu vya maarifa, na karibu na kile tunachoweza na tusichoweza kwa njia ya msaada;
- utayari wa kuunganisha jamii na wadau wengine wa nje kama inavyotakiwa.

### KUSHIRIKI

**AWALI** Matumizi yanjia tofauti za kushiriki (majadiliano ya kikundi cha utafiti, matembezi ya utafitikatika jamii, kufanya ramani) na uchambuzi mdogo sana kuhusu ufanisi wa mbinu hizo.

Kuwasikiliza watu ili kuelewa mapendeleo yao yanayohusiana na uwasilishaji wa vifaa na huduma za WASH, lakini sio lazima kutumia muundo ipasavyo.

Kushauriana na vikundi tofauti kuhusu mahitaji na upendeleo wao lakini sio kwa njia thabiti au yenye muundo.

**SASA** Uongezeko wa kipimo cha Ushirikiano wa Jamii ili kuelewa ufanisi wa kila mbinu, na kuhamasisha na kuunga mkono mabadiliko ya tabia

za watu. Kufanya kazi na jamii katika muundo shirikishi na marekebisho.

Kushauriana na vikundi anuwai, kuhakikisha kuwa matatizo yao yanashughulikiwa (kwa kutumia mpango na muundo wa vifaa vya WASH vilivyobadilishwa ipasavyo), na kisha kushauriana tena: SHAURIANA. BADILISHA, SHAURIANA.

### UFAHAMU

**AWALI** Kufanya majaribio marefu ya maarifa,, mtazamo na kutumia uchunguzi mwanzoni na mwishoni mwa miradi. Njia hizi hazikuweza kutambua vizuri mabadiliko maalum yanayohitajika,wala kuongeza ufahamu wetu wa matendo na matakwa ya watu.

**SASA** Ufahamu bora wa muktadha – kwa msingi unaoendelea kwa kutumia njia msingi yakinifu – kutambua wadau rasmi na wasio rasmi, vyanzo vya habari na watoa huduma wa kuaminika katika kiwango cha jamii.

## VIDOKEZO VYA MIPANGO

### Rasilimali Zinazohitajika

Ni muhimu tuendelee kukabiliana na mipango yetu ya WASH kwa njia ambayo inashirikisha CE kikamilifu — hii inahitaji kubaini rasilimali muhimu kulingana na mpango, kutambua mapungufu katika uwezo, na kurekebisha miongozo ya bajeti ipasavyo.

### WAHUDUMU
**Rasilimali ya Watu**

Uwekezaji ulioongezeka katika rasilimali ya watu, hasa katika kiwango cha nyanja ya kitaaluma (kutangamana na jamii).

**MIFANO**
- ***Watu 500 waliolengwa:*** *Mtu 1 Aliyejitolea wa Jamii wa PHP/WASH (CBV)*
- ***Watu 5,000 waliolengwa:*** *Kama ilivyo hapo juu, pamoja na Msaidizi 1 wa PHP (yaani Msaidizi 1 wa PHP, CBV 10)*
- ***Watu 10,000 waliolengwa:*** *Kama ilivyo hapo juu, pamoja na Afisa 1 wa PHP (yaani Afisa 1 wa PHP, Wasaidizi 2 wa PHP, CBV 20)*
- ***Watu 30,000 waliolengwa:*** *Kama ilivyo hapo juu, Kiongozi 1 wa Timu ya PHP (yaani TL 1 wa PHP, Afisa 3 wa PHP, Wasaidizi 6 wa PHP, CBV 60)*
- ***Watu zaidi ya 50,000 waliolengwa:*** *kama ilivyo hapo juu, pamoja na mratibu 1 wa PHP, wanaohitajika wa huduma maeneo mbalimbali ya ofisi za nje, milipuko, au makabiliano magumu zaidi*
- *Afisa wa Maelezo ya WASH / Kuripoti / Mawasiliano*
- *Msaada wa wataalamu kulingana na muktadha: mtaalam wa magonjwa ya mlipuko/mwana anthropolojia*

### UWEZO
**Ufahamu na Ujuzi**

- Ufahamu na ustadi wa kushirikisha jamii ifaavyo.
- Mafunzo/ukuzaji wa uwezo

**MIFANO**
- *Ukuzaji wa uwezo wa WASH*
- *Miongozo na vifaa vya CE vilivyobadilishwa kulingana na muktadha*
- *Viashiria katika mfumo wa kimantiki*

### BAJETI
**Rasilimali za Kifedha**

- Miongozo ya bajeti inayoweza kubadilika
- Miongozo maalum ya bajeti

**MIFANO**
- *Ruzuku za Jamii kwa ajili ya mawasiliano ya ziada/bonasi ya simu, usafiri, vifaa, mafunzo n.k.*
- *Utafiti wa uchambuzi (km. uchunguzi wa anthropolojia katika maambukizi ya magonjwa)*
- *Msaada wa lugha (Watafsiri bila Mipaka: utafiti wa lugha na mafunzo ya mawasiliano ya tamaduni mbalimbali)*
- *Kukusanya, kuchambua na kutumia kwa utaratibu maelezo yakinifu. K.m. Kifuatilia Mitazamo ya Jamii*